

MIFANO YA HALI YA UBAGUZI WA JAMII

- Kukataa kufanya marekebisho au udumishaji kwa mpangaji kwa sababu wewe ni mkimbizi.
- Mwenye nyumba anadai kuwa chumba/fleti haipo wakati unapodhani hataki kukupangisha wewe kwa sababu ya jamii, rangi na asili ya taifa lako. Kwa mfano, pale unapoenda wewe mwenyewe, mwenye nyumba anaweza kusema “Samahani, lakini baada ya kuzungumza kwenye simu, tulipangisha sehemu iliyobaki.”
- Akikuelekeza kwenye au kutoka kwenye jamii fulani: “Labda ungeweza kujisikia vizuri zaidi katika eneo tofauti la ujirani.”
- Anataka kwamba wapangaji wote wazungumze Kiingereza.
- Anakwambia kwamba huwezi kupika chakula fulani kinachohusiana na utamaduni wako kwa sababu ya harufu yake



JE, UNATAKA USHAURI AU TAARIFA KUHUSU SHERIA YA MAKAZI SAWA?

Zungumza na mwanasheria bila malipo kwa kuwapigia Idaho Legal Aid's Housing Advice Line kwa simu **208-746-7541** Jumatatu-Ijumaa saa 04 asubuhi hadi saa 09:30 Alasiri MST (kwa TRS, piga 7-1-1).

Kwa majaribio, lipigie simu Baraza Makazi Sawa la Intermountain: 208-383-0695 au 1-800-717-0695.

UNAHITAJI KUWASILISHA MALALAMIKO YA FHA?

Wasiliana na HUD kwa 1-800-669-9777 au 1-800-927-9275 (TTY) au tembelea hud.gov/fairhousing

Kwa taarifa zaidi kuhusu haki zako za Sheria ya Makazi Sawa:

hud.gov/fairhousing
idaholegalaid.org
ihfciidaho.org
208-746-7541

Kazi ambayo imetoa msingi wa chapisho hili ilisaidiwa kwa fedha chini ya ruzuku ya Idara ya Makazi na Maendeleo ya Miji ya Marekani. Kiini na matokeo ya utafiti huu yanawekwa kwa ajili ya matumizi ya umma. Mwandishi na mchapishaji wana dhamana ya usahihi wa maelezo na tafsiri iliyopo katika chapisho hili. Tafsiri hiyo si lazima iakisi mitazamo ya Serikali.

Makazi Sawa: Jamii, Rangi, na Asili ya Taifa



Idaho Legal Aid Services, Inc.

SHERIA YA MAKAZI SAWA

Sheria ya Makazi Sawa inakataza ubaguzi katika uuzaji na upangishaji wa makazi kwa misingi ya: Jamii, Rangi Jinsia, Dini, Asili ya Taifa, Ulemavu, au Hali ya Kijamii ya mtu. Ilipitishwa kama sehemu ya Sheria ya Haki za Raia ya 1968.

Sheria ya Makazi Sawa inaweza kutumika kwa watangazaji, wenye nyumba, wasimamizi wa nyumba, wamiliki wa nyumba, HOA, mawakala wa viwanja, mabenki/viongozi, na wengine.

Sheria ya Makazi Sawa inakataza ubaguzi kulingana na tabaka linalolindwa, kama vile: kukataa kumpangisha mtu kwa sababu ya dini yake, kumfukuza mpangaji kwa sababu sio raia wa Marekani, au kutangaza kwamba sehemu inapangishwa kwa wapangaji ambao wanzungumza Kiingereza.



Kwa taarifa zaidi, tembelea hud.gov

JAMII, RANGI, ASILI YA KITAIFA

Kukataa kupangisha, kufukuza mpangaji, kukataa kuuza, kuelekeza au kubagua, kukataa kukopesha, au utofauti wa ushughulikiaji kulingana na jamii au rangi ya mtu kunakiuka katazo la Sheria ya Makazi Sawa dhidi ya ubaguzi wa jamii & rangi (rangi ya ngozi). Ingawa Sheria ya Makazi Sawa ilipitishwa zaidi miaka 50 iliyopita, ubaguzi wa makazi kwa misingi ya jamii & rangi bado upo hadi sasa.

Asili ya Taifa ikiwemo: sehemu ya kuzaliwa, kabila, ukoo, utamaduni, lugha, & lafudhi. Kila mtu analindwa na Sheria ya Makazi Sawa, bila kujali hadhi ya ukimbizi. Hauwezi kunyimwa makazi kwa sababu wewe au familia yako ni kutoka nchi nyingine, una jina au lafudhi inayohusiana na kundi la asili ya taifa fulani, au kwa sababu unafuata mila fulani.

Ubaguzi kwa misingi ya jamii, rangi, au asili ya taifa mara nyingi ni vigumu kubainika, hivyo waathirika hawawezi kujua kwamba sababu iliyofanya wanyimwe makazi, wapandishiwe gharama, au kuelekezwa kwenye sehemu fulani ni kutokana na hadhi maalum. Ikiwa unadhani unatendewa tofauti kwa sababu ya jamii, rangi au asili ya taifa lako, wasiliana na Idaho Legal Aid Services au HUD kwa msaada.

